TANGAZO LA SERIKALI Na. 815 la tarehe. 20/9/2024

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

SHERIA NDOGO YA USHURU WA MAZAO YA UVUVI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KALAMBO YA MWAKA, 2024

Jina

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ushuru wa Mazao ya Uvuvi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

Sura 279

"Afisa Uvuvi" maana yake ni Afisa Uvuvi yeyote anayetambulika na Sheria ya Uvuvi mwenye dhamana ya kuandikisha vyombo vya uvuvi, wavuvi, wachuuzi wa samaki pamoja na bidhaa zitokanazo na samaki katika eneo la Halmashauri;

"Kitengo cha Usimamizi wa Mialo" maana yake ni kitengo kinachohusika na usimamizi wa rasilimali za uvuvi;

"chombo cha uchukuzi" maana yake ni chombo chochote cha usafiri wa majini au nchi kavu kilichotengenezwa maalum kwa kutumika kubeba, kusafirisha au kuchukua samaki wakavu, wabichi kwa kutumia vibebea barafu na chombo hiki chaweza kuwa gari, boti, karua, kilagala, ngama, mashua ya kutumia injini, mashua, mtumbwi wa kutumia joshi au kasia; na chombo hicho kiwe

kimesajiliwa na Shirika la Uwakala wa Meli Tanzani;

"chombo cha uvuvi" maana yake ni mtumbwi au chombo chochote kilichosajiliwa au kukatiwa leseni kwa ajili ya shughuli za uvuvi;

"dandali" maana yake ni vipande viwili vya fito vilivyotengenezwa kwa duara au namna nyingine yoyote na kusukwa kwa kamba na miti, katani au manila na hutumika kufungia samaki wakavu wakati wa kusafirisha kwenda kuwauza;

"Halmashauri" Maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo au Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Mwalo" maana yake ni kando kando ya Ziwa, bwawa au sehemu yoyote ile inayotumiwa na wavuvi kutua, kupakua au kupakia samaki na zana za uvuvi na bidhaa nyinginezo kwa madhumuni ya biashara au matumizi ya nyumbani;

"sumu" maana yake ni madawa yatokanayo na miti au yanayoweza kutengenezwa viwandani ambayo hutumika kwa kuwaleweshea au kuwaua samaki ;

"Wakala" maana yake ni kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Ushuru wa mazao yatokanayo na uvuvi

4.-(1) Halmashauri itatoza ushuru kwa mazao yanayotokana na uvuvi ndani ya Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Mazao ya uvuvi yatakayoingizwa ndani ya Halmashauri kwa madhumuni ya biashara yatalipiwa ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Kibali cha kukusanya ushuru

5.-(1) Mtu binafsi, kampuni au taasisi yenye lengo la kukusanya ushuru wa mazao ya uvuvi kwenye Halmashauri kwa kutumia mashua, mtumbwi, karua, ngama, gari au kwa kutumia sanduku la kuhifadhia samaki atatakiwa kuomba kibali kwa Mkurugenzi kwa kujaza

fomu maalumu na kusaini mkataba kama ilivyobanishwa katika Jedwali la Pili .

(2) Mtu binafsi, kampuni au taasisi ambayo maombi yake yamekubaliwa atapewa kibali na Halmashauri kama ilivyobainisha katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hii.

(3) Ushuru wa Mazao ya Uvuvi utakusanywa na Afisa Mwidhiniwa, au wakala wa Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(4) Kila mmiliki wa chombo cha uvuvi au mwakilishi atapaswa kutoa ushirikiano kwa Afisa Mwidhiniwa au Wakala wa Halmashauri na kuhakikisha kuwa Ushuru wa Mazao ya Uvuvi unalipwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(5) Mtu yeyote aliyelipia ushuru wa samaki na mazao yake atatakiwa kuonyesha stakabadhi ya kielektroniki endapo atahitajika kufanya hivyo kwa ajili ya uhakiki na ukaguzi.

Sehemu zisizo ruhusiwa kuuza, kununua na kusafirisha mazao ya uvuvi

6. Halmashauri itaainisha sehemu zisizo ruhusiwa kuuza, kununua na kusafirisha mazao ya uvuvi.

Ushuru wa kusafirisha mazao ya uvuvi

7.-(1) Mtu yeyote atatakiwa kuwa na kibali na kulipia ushuru wa mazao ya uvuvi kwa Halmashauri kabla ya kusafirisha.

(2) Endapo mtu yeyote atasafirisha mazao ya uvuvi bila kulipa ushuru atatakiwa kulipia asilimia hamsini ya anachodaiwa ikiwa ni kufidia gharama za kufuatilia ushuru huo.

Kipindi maalumu cha kusimamisha shughuli za Uvuvi

8. Halmashauri itatangaza kipindi maalumu cha kusimamisha shughuli za uvuvi ili kupisha samaki kuzaliana.

(a) Mtu yeyote hatoruhusiwa kuvua samaki katika kipindi ambacho shughuli za uvuvi zitakuwa zimesimamishwa.

*Tangazo la Serikali Na.815 (Linaendelea.)*

Usajili wa vyombo vya uvuvi

9.-(1) Halmashauri itasajili vyombo vya uvuvi na kuvipatia namba za usajili.

(2) Chombo ambacho kitafanya shughuli za uvuvi bila kusajiliwa, mmiliki wa chombo hicho atakuwa ametenda kosa na atatakiwa kukisajili na kulipa faini ya asilimia hamsini ya ushuru ili kufidia gharama za ufuatiliaji.

(3) Endapo mmiliki wa chombo hicho atashindwa kulipia chombo chake ndani ya saa ishirini na nne toka kilipokamatwa na Halmashauri au Wakala, chombo hicho kitataifishwa na kuuzwa kwa mnada ili kufidia gharama pamoja na ushuru baada ya kupata amri ya Mahakama.

Marufuku ya kutojirudia kwa namba ya usajili

10.-(1) Chombo chochote cha uvuvi hakitatakiwa kujirudia namba ya usajili.

(2) Endapo itakapobainika kuwa chombo au vyombo vya uvuvi au usafiri wa majini umejirudia namba ya usajili Halmashauri itataifisha vyombo vyote ambavyo vimejirudia namba na itaviuza kwa mnada wa hadhara baada ya kupata amri ya Mahakama.

Ada ya Kibali

11. Kibali cha kusafirishia mazao ya uvuvi kitalipiwa shilingi elfu kumi.

Makosa

12. Mtu yeyote-

(a) anayetoka nje ya eneo la Halmashauri na kufanya shughuli za uvuvi bila kuripoti kwa Kitengo cha Usimamizi wa Mialona kupata kibali;

(b) kanayefanya shughuli za ukusanyaji, utengenezaji na usafirishaji wa samaki wabichi, wa kubanikwa kwa moshi, jua au chumvi bila ya kuwa na kibali cha Halmashauri;

(c) anayepakia au kusafirisha mzigo wowote wa samaki, mabondo au bidhaa nyinginezo zitokanazo na mazao ya uvuvi kutoka mwaloni au eneo lolote la Halmashauri bila ya kulipiwa ushuru wa mazao ya uvuvi;

(d) anayevua samaki kwa kutumia nyavu zisizoruhusiwa;

*Tangazo la Serikali Na.815 (Linaendelea.)*

(e) anayevua au kuua samaki wadogo ambao hawajakua kufikia kiwango cha kuvuliwa.
(f) anayefanya shughuli za uvuvi na kusafirisha samaki nyakati za usiku bila ya kulipia ushuru;
(g) anayemzuia, kumgomea au kumshambulia Afisa uvuvi, Afisa Mwidhiniwa au Wakala wakati anapotekeleza mojawapo ya majukumu yao;
(h) anayefanya biashara ya uvuvi au kuuza samaki au mazao yatokanayo na samaki bila leseni;
(i) anayesafirisha samaki wabichi ambao watathibitika wana madhara kwa mlaji.
(j) anayelima mazao ya chakula ndani ya ziwa na matumizi ya dawa zenye sumu za magugu na wadudu;
(k) anayeuuza samaki wabichi na wakavu katika maeneo yasiyoruhusiwa kama barabarani bila kujali afya ya mlaji.

Adhabu

13. Mtu yeyote anayekiuka masharti ya kifungu chochote cha Sheria Ndogo hii anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na kisichozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote.

Kufililisha kosa

14. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufililisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Nne la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

*Tangazo la Serikali Na.815 (Linaendelea.)*

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 4 (1)*

USHURU WA MAZAO YATOKANAYO NA UVUVI

| MAZAO YA UVUVI | UJAZO | KIASI CHA USHURU<br><br>Tshs |
|---|---|---|
| Perege<br><br>Kambale<br>Kuhe<br>Sato<br>Sangara<br>Migebuka | Kilo 1 | 100/= |
| Dagaa | Kilo 1 | 100/= |
| Samaki wa mapambo | Kwa Samaki | 300/= |

________

JEDWALI LA PILI

________

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 5(1*

KIBALI CHA KUKUSANYA USHURU

Picha ya Mwombaji

Namba ya Leseni ……………………… Namba ya Simu……………………….

Kibali hikikinatolewa kwa Bwana/Bibi/Bi./Ndugu………………………………..…………

ambaye ni mkazi wa……...…………………. Wilaya ya……………………………… Mkoa wa ………………………………………………. kufanya shughuli za uvuvi/ununuzi/ usafirishaji wa Samaki kutoka eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo.

Kibali hiki kitatumika kuanzia tarehe ……. mwezi wa ……… Mwaka …….…….

Mpaka tarehe ………………. Mwezi ……………………… mwaka ……………

Mwombaji wa kibali amelipa malipo yote yanayohusiana na kibali hiki kwa stakabadhi Na…………………………… ya tarehe ……..mwezi …………….. mwaka……….

……………………………………………..

Afisa Uvuvi (W)

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 5(2)*

KIBALI CHA KUSAFIRISHA MAZAO YA UVUVI

Kibali kinatolewa kwa Bwana/Bibi/Bi/Ndugu ……………………..…..……………… ambaye anamiliki leseni ya biashara Na. ……….…………………. ya kusafirisha samaki/mazao ya uvuvi. Bidhaa zitokanazo na samaki kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo kwenda sehemu iliyobainishwa hapa chini kwa ajili ya biashara au matumizi ya nyumbani.

| Na. | Aina ya Samaki | Idadi ya Mzigo | Kizio | Thamani yake | Kituo anakopeleka | Ada iliyolipwa kwa Halmashauri |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | | |
| 2. | | | | | | |
| 3. | | | | | | |

Tarehe ambayo kibali kimetolewa ………...………………………..………………………………
Tarehe ya mwisho wa kibali ……………………………………...………………….……………..

……………………
Afisa Uvuvi (W)

………..…………………
Saini ya Mwombaji wa Kibali

*Tangazo la Serikali Na.815 (Linaendelea.)*

JEDWALI LA NNE

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 14)*

FOMU YA KUFILILISHA KOSA

Mimi …………………………..……………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………………………. ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Kalambo, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya Kifungu cha …… cha Sheria Ndogo ya Ushuru wa Mazao ya Uvuvi ya mwaka, 2024.
Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo, Niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.
NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………. ya mwezi…………..… mwaka …………….
Jina………………………………..
Saini………………………
Mbele yangu :
Jina: …………………………………..……………
Saini……………………….…………………………
Wadhifa: ………………………………………………
Tarehe……………………………………………………

*Tangazo la Serikali Na.815 (Linaendelea.)*

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo imegongwa kwenye Sheria Ndogo hii kufuatia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo uliofanyika tarehe 4/11/2022 na kushuhudiwa lakiri hiyo ikigongwa mbele ya:-

SHAFI K. MPENDA,
*Mkurugenzi mtendaji,*
*Halmashauri ya wilaya,*
*Kalambo*

DAUDI NZELANI SECHOME,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya wilaya,*
*Kalambo*

L.S

NAKUBALI,

Dodoma,
19 Julai, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB.)
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*,